

Mitazamo ya Waafrika kuhusu Urithishwaji wa Mali: Uchunguzi wa Bunilizi za Kiswahili

Martina Duwe na Adria Fuluge
Chuo Kikuu Mzumbe

Ikisiri

Kurithisha mali katika jamii nyingi za Kiafrika ni suala linalohifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii. Hivyo, thamani ya mwanadamu katika ulimwengu wake hubainika pia kupitia mali anazorithisha wengine. Vilevile, kupitia mali hizo, mrithishaji anaendelea kuishi katika fikra za wanaorithishwa hata baada ya kifo chake. Kwa msingi huo, urithishwaji wa mali ni hazina inayoendeleza kizazi na kuleta kumbukumbu idumuyo katika ulimwengu halisi wa mwanadamu. Fasihi ni akiso la maisha ya mwanadamu katika mazingira yake halisi. Kwa mantiki hiyo, bunilizi za Kiswahili huhifadhi na kudokeza misingi mbalimbali inayozingatiwa katika kuendesha maisha ya jamii. Mathalani, ile inayohusu suala la urithishwaji wa mali kupitia wahusika wanaosukwa kwa ustadi unaokidhi haja ya kufikisha maudhui lengwa. Hata hivyo, haijielezwa bayana mitazamo ya Waafrika kuhusu suala la urithishwaji wa mali kwa kuhusianisha na bunilizi za Kiswahili. Hivyo basi, makala hii imeshughulikia jambo hilo kwa kujiegemeza katika riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975). Makala hii ni matokeo ya data zilizopatikana maktabani kwa kutumia mbinu ya usomaji. Vilevile, katika uchunguzi, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo hayo, misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi imetumika. Matokeo yanaonesha kuwa katika suala la urithishwaji wa mali kwa Waafrika, kuna mitazamo mbalimbali inayozingatiwa. Makala hii inajadili mitazamo mikuu mitatu, ambayo ni: mtazamo wa kitamaduni, kihari, na kimabavu.

Istilahi Muhimu: *Bunilizi, Urithi, na Mali, Urithishwaji Mali*

Utangulizi

Bunilizi ni masimulizi ya kihadithi yanayofafanua masuala fulani ya kijamii kwa mtiririko uliobuniwa na msanii. Mtiririko huo hukamilishwa na wahusika wanaobeba uhusika wa hali, tabia, uwezo au matendo fulani katika kuwasilisha maudhui lengwa (Mulokozi, 2017). Hivyo, wahusika waliopo katika bunilizi huakisi maisha halisi ya jamii kwa matendo na hali zao. Kimsingi, pamoja na kazi za kibunilizi kulenga kutoa burudani kwa mwanadamu anayezitazama na kuzisoma kazi hizo, pia, hulenga kuboresha na kurekebisha tabia za jamii kupitia uhusika wa wahusika wa kazi lengwa (Mlacha na Madumulla, 1991). Sambamba na hayo, bunilizi za Kiswahili huhifadhi na kuonesha utajiri wa maarifa yanayoisawiri jamii husika. Miongoni mwa maarifa hayo ni yale yanayohusu mitazamo ya Waafrika kuhusu urithishwaji wa mali.

Urithi ni mali na vitu vingine vyote vilivyochwa na mtu aliyefariki dunia ili vigawiwe kwa wanawe na ndugu zake wa karibu (BAKITA, 2017). Sambamba na fasili hiyo, Swai (2021) anaeleza kwamba mtu anaweza kugawa mali alizonazo kwa ndugu zake kwa ridhaa yake kabla hajakutwa na umauti. Kwa mantiki hiyo, makala hii inajadili dhana ya urithi kama mchakato wa ugawaji wa mali unaofanywa na mwenye mali kabla hajafariki au ndugu baada ya mwenye mali kufariki. Mali zinazogawiwa baada ya mwenye mali kufariki hujulikana kwa jina la mirathi. Kimsingi, mirathi ni mali iliyoachwa na marehemu kwa ajili ya kurithishwa warithi wake halali. Sheria ya nchi, hususani Tanzania imeweka taratibu maalumu zinazoongoza ukusanyaji, uangalizi, usimamizi, ugawaji na umiliki wa mali za marehemu (National Organisation for Legal Assistance, 2006). Katika jamii za Kiafrika, mchakato wa urithishwaji wa mali hujiegemeza katika mitazamo fulani ya utekelezaji wa jambo hilo. Tangu enzi za mababu, mwanadamu alirithi na kurithisha vitu vya thamani kwa kizazi kingine. Hivyo, suala la urithishwaji wa mali halina ukomo katika duara ya maisha ya mwanadamu. Kwa kuzingatia hilo, kila akifanyacho mwanadamu katika ulimwengu wake halisi ni maandalizi ya

kurithisha kizazi chake na jamii kwa jumla. Vilevile, mtu huweza kurithishwa jambo fulani kwa kupenda au kutopenda. Hii ni kutokana na mtazamo wa mrithishaji au warithishaji kuhusu mwenendo, uwezo au tabia za mrithishwaji. Zaidi ya hayo, siyo kila kitu au jambo analirithi mtu katika jamii yake linaweza kuwa na manufaa kwake (Kezilahabi, 1985). Kwa jumla, ni hulka ya mwanadamu kuona anarithishwa mali za wazazi wake kama vile nyumba, mashamba na hata biashara. Wengine hurithishwa pesa zilizowekwa kwenye akaunti za wazazi wao. Hivyo, urithishwaji wa mali ni mchakato unaohusisha utoaji wa mali fulani ya mtu na kupewa mtu mwingine.

Mali ni vitu vyenye thamani kubwa alivyonavyo mtu (TUKI, 2014). Vitu vya thamani katika mazingira halisi ya Waafrika hutegemea mtazamo wao juu ya kipi chenye thamani kwao kwa kuzingatia kufaa kwake. Kwao, masuala yote yanayoenzi na kuhifadhi amali za jamii hutazamwa kwa thamani ya pekee na hurithishwa kizazi kimoja hadi kingine. Hapa tunaweza kugawa vitu vyenye thamani kwa Waafrika katika makundi makuu mawili. Kwanza, visivyoonekana kwa macho lakini huthaminiwa na huendelea kurithishwa kwa kuwa vina manufaa katika ustawi wa maisha yao. Mathalani, kwa Waafrika masuala ya kiimani yana thamani inayokitwa katika misingi ya mila na desturi zao kama vile, uganga, uchawi na matambiko. Masuala haya ni miongoni mwa amali za jamii za Waafrika kwa kuwa hudhihirisha falsafa yao na hurithishwa kwa namna inayokidhi misingi ya tamaduni zao (Idowu, 1973). Mapokeo ya urithishwaji wa maarifa haya, hubainika kupitia matendo yao ya kila siku.

Sambamba na hayo, maarifa kama vile, hekima na busara, upendo na unyenyekevu, utii na uvumilivu na malezi kwa Waafrika huenziwa kwa thamani kubwa na hurithishwa katika mzunguko wa maisha ya kila siku. Masuala haya yote ni tunu za maisha bora ya Waafrika na hurithishwa kulingana na miongozo inayozingatiwa katika jamii husika (Oruka, 1990). Kwa jumla, urithishwaji wa maarifa haya hulenga kuiandaa jamii kuishi vema katika mazingira yao na kuendeleza mila na desturi za jamii kama methali isemavyo, *mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo*. Hivyo, maarifa mema ni kitu cha thamani kwa Waafrika ambapo huendelea kurithishwa kizazi kimoja hadi kingine. Kwa msingi huo, dhana ya mali inaweza kufafanuliwa kuwa ni ujuzi au maarifa ayapatayo mtu yatakayomfaa maishani mwake. Mathalani, kumthirisha mtoto maarifa yanayosawiri utamaduni wa jamii yake ni urithi bora kwa kuwa maarifa hayo humsaidia kupambanua jema na baya na kuzingatia vema misingi ya kaida za jamii. Kwa jumla, mchakato mzima wa kulea familia ni urithishwaji wa maarifa yanayohusu masuala mbalimbali kulingana na utamaduni wa jamii.

Pili, mwanadamu huweza kurithi vitu vya thamani vinavyoonekana dhahiri kama vile, mifugo, ardhi, pesa na majumba. Hizi ni mali zinazoweza kurithishwa na mhusika kabla ya kufa kwake kwa walengwa wa mali hizo. Vilevile, baada ya kufariki kwa mwenye mali, familia au ndugu hurithi kwa kuzingatia misingi inayoonekana kufaa katika mchakato wa kuzigawa mali hizo. Hivyo, makala hii inajikita katika kufafanua misingi inayozingatiwa katika urithishwaji wa mali zinazodhihirika bayana. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mali hizi hutokana na juhudi za mtu katika kufanya kazi na huchukuliwa kama msingi wa kuendesha maisha ya mwanadamu. Kwa mantiki hiyo, siyo watu wote katika maisha yao wanafanikiwa kuwa na mali zitakazorithishwa kwa watoto au ndugu zao. Vilevile, mali hizi ndizo zinazoleta mitazamo tofautitofauti ya namna ya kurithi ambapo athari yake hubainika kupitia mchakato wa urithishwaji wake. Kiuhalisi, kila mwanadamu anatamani kuona na kumiliki vitu vya thamani vinavyoweza kumpa heshima katika jamii yake (Idowu, 1973). Kwa hivyo, panapotokea kutoa maamuzi kuhusu misingi ipi itumike kugawana mali zilizoachwa na mtu fulani, kila mmoja hujiegemeza katika mtazamo wake kulingana na mapendeleo yake kama Waswahili wasemavyo *kila mwamba ngoma, ngozi huvutia kwake*. Kwa msingi huo, makala hii inashughulikia mitazamo ya Waafrika kuhusu urithishwaji wa mali kwa kujiegemeza katika riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975).

Muhtasari wa Riwaya Teule

Rosa Mistika (ua waridi lenye fumbo) ni riwaya ya kijamii iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi mwaka 1971. Inaitwa riwaya ya kijamii kwa sababu inaakisi uhalisi wa mazingira mahususi ya kijamii. Hii ndiyo kazi ya kwanza kuandikwa na mwandishi huyu na ndiyo iliyomtambulisha kama mwandishi stadi katika uga wa riwaya ya Kiswahili. Katika riwaya hii, mwandishi anaonesha picha ya kipindi ambacho waandishi walianza kuzama katika kuhakiki uhalisi wa mambo katika jamii. Suala hili linathibitika kupitia mhusika wake mkuu, Rosa Mistika, ambaye anaishia katika tanzia. Kwa jumla, mwandishi anaonesha jinsi malezi ya ukali na kukandamizwa kwa uhuru wa watoto yanavyochangia kuwaangamiza watoto hao badala ya kuwajenga vizuri. Mulokozi (1983) anaeleza kuwa mhusika mkuu, Rosa, ni kielelezo cha dhamiri hiyo inayoonesha kuwa mazingira na siyo roho, fikra au uadilifu wa mtu, ndiyo humjenga mtu. Mambo mengine yanayodokezwa na mwandishi katika riwaya yake ni pamoja na matabaka katika jamii, athari za urithishwaji wa mali na ulevi wa kupindukia.

Kwa upande mwingine, *Dunia Uwanja wa Fujo* ni riwaya iliyoandikwa pia na Euphrase Kezilahabi mwaka 1975. Hii ni riwaya ya kisiasa inayoelezea kufutika na kutokufikiwa kwa ndoto ya matarajio ya Watanzania kuhusu kuifikia nchi ya ahadi ya Azimio la Arusha. Katika riwaya hii, mwandishi anaonesha namna hali ya uchumi ilivyoanza kudidimia waziwazi kutokana na uroho, usaliti na rushwa ya viongozi wa serikali miaka ya 1970. Katika kipindi hicho, tapo la uhalisia wa kihakiki lilizidi kupevuka. Aidha, mkondo wa kidhanaishi ulizidi kupata mashiko kutoka kwa mwasisi wake, Kezilahabi, katika riwaya ya Kiswahili (Mlacha na Madumulla 1991). Kwa jumla, katika riwaya hii ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, Kezilahabi anaukuza mkondo wa uhakiki wa kiteti kwa kasi kubwa zaidi kwani analitazama suala la maisha kifalsafa kwa karibu zaidi. Mwandishi huyu kupitia riwaya hii anayaona maisha kama kitu kilicho katika mvurugano usio na ulinganifu, na kwamba ndivyo maisha yanavyopaswa kuwa na kueleweka; kwamba ni mchafuko au vurugu tupu. Wafula (2002) anaeleza kuwa katika riwaya hii, Kezilahabi anaonesha udhanifu uliokithiri na ukosefu wa dira na namna sera ya ujamaa na kujitegemea ilivyoenezwa kwa watu. Anaendelea kueleza kuwa Kezilahabi analaumu namna sera ilivyoenezwa hasa kutokana na kutokutolewa kwa elimu yoyote kwa ngazi ya chini katika maandalizi ya sera hii mpya ya uchumi, sera ya ujamaa na kujitegemea, na pia kutoandaliwa kwa viongozi wa chama waliokuwa wakiihubiri sera hiyo. Hivyo, riwaya hii, imeshughulikia matatizo na mikinzano mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kifalsafa. Kutokana na mikinzano hiyo, dhamira mbalimbali zinaibuliwa.

Kiunzi cha Nadharia

Mchakato wa upatikanaji wa matokeo haya uliongozwa na misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi. Coser (1963) anaeleza kwamba nadharia hii iliasisiwa na Charles Taylor (1822 - 1917) na kuendelezwa na Hippolyte Taine (1828 - 1893) na George Lukacs (1885 - 1971). Katika uchunguzi wake, Taine aliangalia kazi ya fasihi kama taswira ya kijiografia, kitamaduni na kimazingira iliyochimbuka kutoka katika jamii husika. Kwa upande wake, Lukacs anaeleza kwamba mambo mbalimbali ya kijamii yanayohusiana na uumbaji wa kazi za fasihi, kwa kiasi kikubwa, hutegemea namna mwandishi anavyofungamana na maisha ya jamii husika. Kwa jumla, Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi huelezea sababu za kuibuka kwa kazi fulani ya kisanaa yenye umbo fulani la kijamii, ikiwamo namna fikra za mwandishi zinavyoongozwa na mila, desturi na maisha ya jamii yake. Aidha, nadharia hii huchunguza jinsi mtunzi wa kazi ya kifasihi anavyoathiriwa na tabaka lake, itikadi yake ya kijamii, mazingira ya kiuchumi ya kazi yake, na hali ya jamii anayoilenga. Hivyo, makala hii imejiegemeza zaidi katika mihimili miwili ya nadharia hii, ambayo ni: Mosi, fasihi haiwezi kujitenga na jamii, ambayo, kwayo imeumbwa (Narizvi, 1982). Pili, kazi ya kifasihi ni taswira ya kijiografia, kimazingira, na kiutamaduni, ambamo, kwayo imechimbuka (Mungah, 1999). Mihimili hii imetusaidia kujadili namna mwandishi wa riwaya teule anavyoliangalia suala la urithishwaji wa mali na namna linavyofungamana na maisha ya jamii ya Waafrika kwa jumla. Aidha, data zilizopatikana katika riwaya teule zimetuwezesha kupata picha halisi ya maisha ya jamii ya mwandishi na namna wanavyoishi katika mazingira yao halisi. Hii inatokana na ukweli kwamba mhakiki hawezi kuhakiki kazi yoyote ya fasihi pasipo kuzingatia miktadha ya maisha ya mwandishi.

Methodolojia ya Utafiti

Makala hii imetokana na utafiti uliofanyika katika mwegamo wa kitaamuli. Mwegamo huu humtaka mtafiti kutumia tafakuri ya kina katika kuhusisha taarifa mbalimbali zilizopatikana katika uchunguzi na kutoa ufafanuzi kwa kuzingatia misingi ya nadharia husika pamoja na ithibati bayana (Kothari, 2004). Nao, Merriam & Tisdell (2016) wanasema kwamba utafiti wa kitaamuli hutumia maelezo katika kuwasilisha na kujadili data za utafiti. Wanaendelea kueleza kwamba matokeo ya utafiti yanayopatikana, hutolewa kwa njia ya maelezo na picha zaidi kuliko matumizi ya kimahesabu au takwimu. Kwa kuzingatia hilo, data zilizotoa matokeo haya zilikusanywa maktabani kwa njia ya usomaji wa nyaraka mbalimbali, hususani riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), kisha zilichanganuliwa, kufafanuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo pasipo kuhusisha takwimu. Aidha, uwasilishaji wa matokeo ulihusisha tafakuri binafsi, taarifa mbalimbali za kitafiti, misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi pamoja na data zilizopatikana maktabani.

Matokeo ya Utafiti

Mchakato wa urithishwaji wa mali katika jamii nyingi za Kiafrika huzingatia mitazamo fulani kama miegamo muhimu katika kukamilisha mchakato huo. Kwa mantiki hiyo, hakuna namna moja inayozingatiwa na jamii zote katika mchakato wa urithishwaji wa mali, bali hutegemeana na maamuzi ya wahusika kwamba mtazamo upi utafaa kwa wakati huo. Hivyo, katika makala hii tunamakinikia mitazamo ya kitamaduni, kibinafsi na kimabavu.

Mtazamo wa Kitamaduni

Katika jamii za Kiafrika, urithi na urithishwaji wa mali hutazamwa kama suala la kitamaduni. Urithi na urithishwaji huo, huweza kufanywa na mhusika mwenyewe; yaani, mzazi au mwenye mali akiwa hai kwa mtu au watu anaowataka hususani, watoto. Wakati mwingine hufanywa na ndugu na jamaa baada ya mhusika kufariki. Mara nyingi, urithishwaji wa mali hufanywa kwa kuzingatia mitazamo ya kiutamaduni yenye kujiegemeza katika muktadha wa kijinsi na kiumri.

Kijinsi, uzoefu unaonesha kwamba jamii nyingi za Kiafrika humthamini zaidi mtoto wa kiume kuliko wa kike (Mbiti (1969)). Hivyo, hata suala la urithishwaji wa mali, mtoto wa kiume hupewa kipaumbele zaidi ikilinganishwa na mtoto wa kike. Jambo hili hufanyika bila kuzingatia kama mtoto huyo wa kiume ni wa kwanza kuzaliwa au wa mwisho. Aidha, suala hili linathibitika katika riwaya teule zilizotumika kama chanzo kikuu cha data katika kuandika makala hii ambapo mtoto wa kiume anapewa thamani kubwa zaidi akilinganishwa na watoto wa kike. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) mwandishi anaonesha namna Zakaria anavyoacha ujumbe wa kumrithisha pesa nyingi mtoto wa kiume, Emmanuel, ambaye ni mtoto wa mwisho kuzaliwa huku wale wa kike ambao ni wakubwa kwake wakipewa urithi mdogo. Mwandishi anasema:

Jamaa wengine wa marehemu walibaki ili kugawana vitu vya urithi. Ilijulikana kwamba Zakaria alikuwa bado na shilingi mia saba benki; nazo zilikuwa zimewekwa kwa jina la Emmanuel. Jamaa hawa walimlazimisha Flora aende kuzitoa zile pesa benki waje wazigawane. Flora alipokwenda benki hakuweza kuzipata. Karibu jamaa hawa wawe wehu. Walimwita mwizi, malaya na mshenzi. Jamaa hawa waliona huu ulikuwa mji wa wanawake (uk. 96).

Pamoja na mambo mengine, dondoo hili linadokeza namna jamii ya Zakaria ilivyoamini na kutoa taarifa kuhusu urithi wa mtoto wa kiume wa Zakaria. Swali la kujiuliza ni; je, kwa nini mtoto wa kiume ambaye ni wa mwisho kuzaliwa na siyo Rosa Mistika, mtoto wake wa kwanza kuzaliwa? Hii ni kutokana na ukweli kwamba jamii za Kiafrika zina utamaduni wa kuthamini zaidi watoto wa kiume kuliko wa kike. Kimsingi, mtazamo huu hurithishwa katika fikra za kila mmoja ambapo hata watoto wanapokua katika jamii huanza kujifunza na kupata maarifa ya tofauti zao kijinsia. Hivyo, katika masuala mbalimbali yakiwamo ya urithi, mchakato wake hukuzwa katika akili zao.

Vilevile, matokeo yanaonesha kuwa wapo baadhi ya wazazi wa kiume ambao hufikia hatua ya kuwagombeza au kuwalaumu wake zao wanaposhindwa kuwazalia watoto wa kiume. Uamuzi wa kumtupia mwanamke lawama hizo husababishwa na tafakuri juu ya nani atakayerithi mali za familia.

Mwandishi anabainisha haya kupitia bunilizi zake. Mathalani, katika riwaya ya *Rosa Mistika* Zakaria anaelekeza lawama hizo kwa lugha kali na yenye kuumumiza Regina. Mwandishi kupitia sauti yake anasema: “Mshenzi, unanizalia wasichana tu! Unaniletea taabu nyumbani bure tu!” Zakaria alifoka. Regina hakujibu; aliogopa kumdhihaki... (uk. 23). Kimsingi, Regina hakuwa na furaha kutokana na kupewa lawama za kushindwa kuzaa mtoto wa kiume na mumewe. Pamoja na kuwa amezaa watoto watano wa kike, Regina alijitathmini kuwa ni mwenye kukosa kitu muhimu katika maisha yake ambapo akikipata kitaleta furaha na amani kwao. Haya yanathibitishwa na mwandishi anaposema:

Lakini Regina tangu aolewe hakuwa na raha: alikuwa akisumbuliwa na kuteswa na mumewe kwa kosa lisilo lake. Regina alikuwa na watoto watano wasichana; wote wazuri kama yeye. Matumaini yake ya kukaa pamoja na watoto hao kama alivyoambiwa na bwanake yalika katika mimba ya miezi mitano aliyokuwa nayo sasa... siyo mimba peke yake iliyomfanya Regina asimwache bwanake; ilikuwa pia na moyo aliokuwa nao juu ya watoto wake. Hakutaka kuachana na watoto hao; bila yeye, mumewe alikuwa hawezi kuwatunza. Mawazo yake yalikuwa juu ya furaha ya watoto wake katika maisha yao ya baadaye (uk. 3).

Kinachojitokeza katika dondoo hilo ni kwamba, Zakaria anafikiria kumwacha Regina kwa sababu ya kumzalia watoto wa kike pekee. Hii ni kutokana na kupitia wakati mgumu wa kufikiria kuhusu mtoto wa kiume atakayemrithisha mali zake. Mashaka na malalamiko ya Zakaria kwa mkewe Regina, ni ithibati mojawapo ya jambo hili. Matokeo yanaonesha kuwa familia ikikosa mtoto wa kiume inaona imepungukiwa kitu cha thamani sana. Hivyo, hufanya juhudi mbalimbali kutafuta mtoto huyo ili awe mrithi wa kwanza wa mali zitakazoachwa. Aidha, imebainika kuwa mtoto wa kiume hutazamwa kwa furaha zaidi kwa kuwa ndiye anyetegemewa kuendeleza ukoo husika kwa kuzingatia tamaduni za jamii. Kinyume chake ni kwamba mtoto wa kike akishaolewa anahama ukoo na kuzaa watoto ambao watakuwa mali ya ukoo uliomuoa. Kwa mantiki hiyo, kurithishwa mali mtoto wa kiume kutaleta mwendelezo wa kumiliki na kutumia mali hizo katika ukoo husika. Mtazamo huu unawafanya wanawake hata kama wana watoto watano, sita au saba wa kike, bado wanalazimika kuendelea kuzaa wakiwa na lengo la kumtafuta mtoto wa kiume. Haya yanabainika katika riwaya ya *Rosa Mistika* ambapo Regina aliendelea kuzaa akiwa na haja ya kupata mtoto wa kiume. Alipofanikiwa kumzaa Emmanuel hakuendelea tena. Kimsingi, kitendo cha Regina kuzaa mtoto wa kiume kilimfurahisha Zakaria. Furaha hiyo ilidhihirika siku aliyozaliwa Emmanuel kwani Zakaria alifurahi na kuleta zawadi nyingi kwa Regina huku akimhakikishia kwamba kuzaliwa kwa mtoto huyo ni mwanzo wa amani na utulivu katika familia hiyo. Dondoo lifuatalo linathibitisha furaha ya Zakaria baada ya Regina kumzalia mtoto wa kiume.

“Regina! Sasa mji huu umekuwa wako.”...

Usiku huo Zakaria aliimba aleluya karibu usiku kucha. Kesho yake alikwenda posta. Mke wake alishangaa kumwona jioni anarudi na vitu vyote alivyokuwa ametaja. Alianza kupata sauti. Alianza kuzungumza kwa furaha. Hata watu wa kijijini waliona ajabu... (kur. 24 – 25).

Nukuu hiyo inathibitisha furaha ya Zakaria baada ya kupata mtoto wa kiume. Emmanuel ni mtoto wa sita kuzaliwa lakini ndiye anayeonekana mwenye thamani kubwa katika familia hiyo. Hii ni kutokana na mtazamo wao kuwa mtoto huyo ndiye atakayerithi mali kwa kiasi kikubwa kulingana na misingi ya tamaduni za. Jambo hili lipo katika mazingira halisi ya Waafrika kama wasemavyo wanasosholojia kuwa kazi za kibunilizi ni akiso la maisha halisi ya jamii husika. Kwa hivyo, thamani ya mtoto wa kiume katika jamii ni suala la kiutamaduni na lipo katika fikra za kila mmoja. Haya yanathibitishwa vema na Shabaan Robert (2013) anayesema kwamba suala la kurithisha mali kwa Waafrika ni muhimu katika jamii. Anaonesha kwamba mtu akikosa mtoto wa kumrithisha mali na utawala, huleta masikitiko katika jamii. Zaidi, anasema: “Ustawi uliofanyika katika nchi hii tangu mwanzo wa ufalme wangu, umeniletea heshima. Lakini ugumba umemeza heshima na utasa umetia wimbi fahari ya Malkia. Sina mtoto wa kurithi kiti changu cha ufalme, kutoa mashauri ya hekima

barazani kama mababu zake (uk. 3). Kwa mantiki hiyo, thamani na heshima ya mwanamke ni kuzaa, hususani watoto wa kiume ambao hutazamwa kama warithi wa baadaye.

Vilevile, katika mtazamo wa kitamaduni, mchakato wa urithishwaji wa mali pia unaweza kuwahusisha viongozi muhimu katika jamii husika, wakiwamo viongozi wa dini inayotawala katika jamii hiyo. Kulingana na BAKITA (2017), dini ni imani ya kiroho inayomfanya binadamu aamini kuwapo kwa Mungu. Kwa msingi huo, dini humsaidia mwanadamu kutenda mambo kwa kumwogopa Mungu ambaye ndiye chimbuko la kila kitu kilichopo duniani. Kwa kuzingatia kwamba suala la urithi lipo katika jamii na linakubalika, viongozi wa dini pia, huwa na mchango katika kusimamia haki ili kuepusha migogoro katika jamii. Suala hili linajitokeza katika riwaya za Kezilahabi ambapo katika uwasilishaji wa maudhui yake, viongozi wa dini wameshirikishwa kama watu muhimu katika kuhakikisha haki inatendeka katika mchakato huo kama ilivyoamriwa na mwenye mali. Haya yanabainika katika riwaya ya *Rosa Mistika* ambapo mwandishi anaonesha kuwa viongozi wa dini nao wanashiriki katika kusimamia urithishwaji wa mali za Zakaria kwa kuzingatia ujumbe ulioachwa na Zakaria kabla ya kifo chake. Anasema:

Wakuu wa dini walikuwepo kuangalia kwamba haki ilikuwa ikitumika. Kijikaratasi kilisema kwamba warithi walikuwa ni watoto tu. Kila mtoto alikuwa amepangiwa vitu vya kurithi. Jamaa walikataa kabisa kwamba huo haukuwa mwandiko wake. Wakuu wa dini walipobisha, walichukua mapanga na kuwafukuza sasa walikuwa huru kutenda lolote (uk. 96).

Kinachojitokeza katika dondoo hilo ni kwamba viongozi wa dini wanathaminiwa na kushirikishwa vema katika masuala mbalimbali ya kijamii. Hii ni kwa sababu wao wanaaminiwa kuwa daima husimamia haki na usawa kulingana na misingi inayowaongoza. Azma yao ni kuona mali za Zakaria zinagawanywa kwa wahusika kama zilivyopangwa pasipo kuathiri amani ya familia hiyo. Kulingana na mtazamo wa wanasosholojia, suala hili ni hai katika mazingira halisi ya Waafrika, kwani viongozi wa dini iwe ya kijadi au zilizoletwa na wageni wanahusishwa katika masuala mbalimbali ya kijamii ili kusimamia na kutetea haki kulingana na miongozo inayozingatia.

Mtazamo wa Kihiriari

Huu ni mtazamo au mwegamo unaohusisha maamuzi ya mtu binafsi kuhusu nani arithishwe mali zake. Vilevile, maamuzi hayo huongozwa na vigezo binafsi vinavyodhaniwa kuwa ni sahihi katika kugawa urithi huo. Vigezo hivyo vinaweza visiwafurahishe wengine, hususani wanaozingatia mtazamo wa kitamaduni kwa kuwa anaweza kurithishwa mtoto wa kike mali nyingi na za thamani kuliko wa kiume. Hivyo, katika mtazamo huu mwenye mali hafungwi na mtazamo wa kitamaduni. Kwa hivyo, humrithisha amtakaye kulingana na matakwa yake. Matokeo yanaonesha kuwa mchakato wa urithishwaji katika mtazamo huu mara nyingi hufanyika kabla ya mwenye mali kufariki. Tafakuri yake juu ya nani arithishwe haizuiliwi wala kupingwa na yeyote. Suala hili linajitokeza katika riwaya za Euphrase Kezilahabi. Tukianza na riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anathibitisha hili kupitia maamuzi ya Zakaria kuhusu ugawaji wa mali zake kwa watoto wake kabla ya kufariki kwake. Alifanya hivyo ili kuepusha mizozo ambayo ingeweza kutokea katika familia yake kuhusu nani apewe mali zipi na kwa kiwango gani. Mwandishi anaeleza kuwa:

Katika sanduku jingine walikuta kijibarua kidogo nacho kilieleza habari yote watu watakaorithi vitu. Zakaria alikiandika zamani... Kijikaratasi kilisema kwamba warithi walikuwa ni watoto tu. Kila mtoto alikuwa amepangiwa vitu vya kurithi... Mle ndani walikuta shilingi hamsini ndani ya bahasha iliyokuwa imeandikwa jina la Regina juu. Katika sanduku jingine walikuta kijibarua kidogo nacho kilieleza habari yote kuhusu watu watakaorithi vitu. Zakaria aliandika zamani (uk. 96).

Dondoo hili linathibitisha kwamba suala la urithi ni la kiutamaduni na linafahamika katika jamii ya mwandishi. Aidha, mwandishi anaonesha kwamba Zakaria anatambua umuhimu wa suala la urithi. Hata hivyo, anaonesha kwamba licha ya suala hili kujulikana, bado huweza kusababisha mizozo na

migogoro katika jamii kama halitaratibiwa vizuri. Kutokana na hilo, anaamua kubainisha wazi nani anapaswa kurithishwa mali zake. Kwa jumla, Zakaria aliamua kugawa kabisa mali zake kimaandishi ili kila mmoja apate kulingana na matakwa yake. Ndiyo maana hata mgawanyo wa mali hizo haukuwa sawa. Vilevile, alifanya hivyo ili kuepuka usumbufu watakaoupata watoto wake wakati wa kugawana mali zake. Kwa msingi huo, Zakaria anaonesha namna jamii inavyoweza kukabiliana na tatizo la urithishwaji wa mali kwa kuacha wosia na taarifa sahihi za watu anaotaka warithishwe mali zake. Funzo kubwa linalobainika kupitia urithishwaji wa mali kwa mtindo huu ni kwamba, maishani, sote tupo safarini ambapo kila mmoja lazima atafikia mwisho wa safari hiyo. Hivyo, kugawa mali mapema kwa familia siyo jambo baya kama wengine wanavyosema kwamba ni uchuro¹, bali ni njia bora yenye kuepusha migogoro ihusuyo mchakato wa ugawanaji au ugawaji wa mali hizo.

Sambamba na hayo, suala la urithishwaji wa mali kwa hiari linathibitika pia katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975). Mwandishi anaonesha namna wazazi katika kuishi kwao, wanavyofikiri kuhusu nini watawarithisha watoto wao. Hivyo, katika mahangaiko yao ya kila siku huandaa na kuhifadhi mali kwa ajili ya kizazi chao. Kwa mfano, tunamwona Kapinga daima akiwaza kuhusu kumrithisha mwanawe mali zake. Mwandishi anasema:

Muyango alipokuwa akifanya kosa la kumpenda Tumaini kupita kiasi, Kapinga alifanya kosa la kujali sana Tumaini atarithi nini. ... Hivyo basi ndivyo Tumaini alivyotunzwa; ndivyo alivyokua ... (kur. 11 - 12).

Katika dondoo hilo, jambo muhimu linalobainika ni kwamba, Kapinga daima alikuwa akifikiria kuhusu kumrithisha mali kwa hiari yake kijana wake wa kwanza aliyeitwa Tumaini. Matarajio na mapendeleo yake ya kumrithisha mali mtoto wake yanabainika kupitia maongezi yake na mkewe na kwa mtoto mwenyewe tangu akiwa mdogo. Hivyo, Tumaini alikua huku akijua kwamba mali za babaye atazirithi mara tu akikua. Kimsingi, kulingana na mtazamo wa Wanasosholojia ya Kifasihi, jambo hili linabainika katika mazingira halisi ya Waafrika ambapo mtu anaweza kuwajulisha watoto wake kuwa nani atarithi nini akiwa mkubwa. Kwa mantiki hiyo, kazi ya kibunilizi ni akiso tu la maisha ya jamii.

Mtazamo wa Kimabavu

Mabavu ni nguvu au mamlaka anayotumia mtu kulazimisha kutendeka kwa jambo analolitaka; shurti (BAKITA, 2017). Kimsingi, huu ni mtazamo anaojiegemeza nao mtu au kikundi cha watu katika kujirithisha mali za ndugu yao. Mara nyingi urithi wa namna hii hufanyika baada ya mwenye mali kufariki ambapo mali zake zinaweza kugawanywa kwa wachache kimabavu. Kwa jumla, mwegamo huu huwanyima haki walengwa wa mali hizo au kutogawana kwa usawa. Mwenye nguvu ndiye mara nyingi hunufaika zaidi na mali hizo pasipo kujali wengine. Jambo hili linabainika katika bunilizi za Kiswahili, ikiwamo riwaya ya *Rosa Mistika*. Mwandishi anaeleza kuwa baada ya kifo cha Zakaria na mkewe, Regina, ndugu wa Zakaria wanakumbwa na uchu wa kurithi mali hizo. Wakiwa katika harakati hizo, wanawazuia na kuwapinga hata viongozi wa dini waliohusishwa katika mchakato huo, ambapo kimsingi, viongozi hao husaidia kulinda amani na kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa kila mmoja. Ndugu wa Zakaria wanaamua kuwafukuza ili kurithi mali hizo kwa nguvu. Matokeo yanaonesha kuwa baada ya kuwafukuza viongozi wa dini, ndugu hao wanaendelea kujirithisha mali za Zakaria pasipokufikiri mustakabali wa watoto wa marehemu. Mwandishi anasema:

Hawa jamaa walirithi. Walirithi hawa jamaa. Walirithi, walirithi. Jamaa waligawana vitu. Walirithi kila kilichokuwa ndani ya nyumba. Walirithi michungwa na miembe. Walirithi migomba yote. Walirithi paka na mbwa. Walirithi majani yaliyokuwa juu ya paa, na miti yote iliyofanya nyumba isimame. Walirithi mashamba yote. Walirithi kuku; walirithi hata mbolea ya ng'ombe. Walirithi. Hawa jamaa, kweli walirithi. Lakini hapakuwa na mtu mmoja aliyeweza kusema

¹ Tukio linaloashiria jambo baya: mkosi, laana, nuksi (BAKITA, 2017)

atamchukua mtoto fulani amtunze. Badala yake walim dai John alipe mahari ili pia wagawane (uk. 96).

Kitendo cha kugawana mali kimabavu, kinachofanywa na ndugu wa Zakaria pasipo kuwafikiria watoto wake, kinawaweka watoto hao katika mazingira magumu. Hii ni kwa sababu hawahusishwi kabisa katika mgao huo na kila wanachogusa wanaambiwa siyo mali yao. Jamaa hao wanajali kugawana mali tu na hakuna hata mmoja wao anayetaka wajaadili kuhusu maisha ya watoto hao yatakavyokuwa. Kimsingi, Zakaria alitambua na kuwafahamu jamaa zake kwamba wangeleta usumbufu kwa familia yake kwa kugombania mali zake. Matokeo yanaonesha kwamba, mara nyingi mwenye mali anapofariki, ndugu zake hugombania mali hizo. Matokeo yake, watoto ambao ni warithi halali hukosa au hupata kidogo sana. Kwa mantiki hiyo, mwandishi wa riwaya hii anaonesha kukerwa na kitendo hicho ndiyo maana analirudiarudia neno ‘walirithi’ ikiwa na maana kwamba hakuna kitu ambacho hawakugawana. Hivyo, anaonesha umuhimu wa kuheshimu na kuzingatia maamuzi ya mwenye mali katika mchakato wa ugawaji wa mali hizo.

Kwa jumla, matokeo yanaonesha kwamba jamii zetu zina changamoto kwani husababisha migogoro inayotokana na mgawanyo wa mali pindi mhusika anapofariki. Mara nyingi ndugu hupora kwa nguvu kwa manufaa yao mali zilizochumwa na mhusika na huwanyima au kuwapa sehemu ndogo ya mali hizo walengwa. Jambo hili linabainika vema katika riwaya ya *Rosa Mistika* ambapo ndugu wa Zakaria baada ya kurithi mali zote, watoto wa marehemu walibaki bila kitu. Walipojaribu kushika kitu chochote kilichoachwa na wazazi wao, waliambiwa siyo mali yao tena. Inaelezwa kwamba:

Baada ya kugawana vitu hivi, watoto walikaa pale nyumbani kwa muda wa siku moja tu. Kila kitu walichogusa waliambiwa si chao. “Pesa zenu zimo benki” walitulizwa (uk. 96).

Nukuu hiyo inaonesha namna ndugu wa Zakaria wanavyogawana mali zilizopaswa kurithishwa kwa watoto wake. Kitendo hicho kinawaweka watoto hao katika mazingira magumu kwani wanakosa makazi na malezi bora. Matokeo yake ni kwamba ndugu wanaendelea kunufaika na mali pasipo kujali hatima ya watoto wa Zakaria. Hatimaye, watoto hao wanapobaini kuwa hali inazidi kuwa ngumu, wanaamua kutafuta msaada kwa wasamaria wema ili wawatunze baadhi yao. Mwandishi anasema: “Flora aliwaomba Masista waliokuwa wakikaa Kagunguli wamsaidie kutunza dada zake kwa muda wa miaka miwili. Hawakukataa: walimwonea huruma” (uk. 96).

Kitendo cha Flora kubeba jukumu kubwa la kuhangaika na kufikiri namna wadogo zake watakavyoishi, kinasikitisha na kufedhehesha jamii. Jambo hili linatokana na ndugu wa marehemu kujirithisha mali wasizostahili na kuwaacha watoto wakihangaika peke yao. Matarajio yetu yangukuwa kuwaona jamaa hao wakigombania namna ya kuwalea watoto hao na siyo kugombania namna ya kupora mali za maraehemu. Washukuriwe Masista wa Kagunguli wanaoona thamani ya watoto hawa na kukubali kuwalea huku ndugu wa Zakaria wakiyafurahia maisha yao kwa mali za dhuluma. Kimsingi, mwandishi anaonesha namna suala la urithishwaji wa mali lilivyo na utata katika jamii ya Zakaria.

Aidha, katika riwaya hii mwandishi anaendelea kueleza kwamba suala hili halitokei kwa jamaa ya Zakaria pekee, bali hata kwa Bigeyo. Huyu anakumbwa na tatizo hili baada ya kufiwa na mumewe, Ndaro, ambapo hakuweza kurithi mali walizochuma na mumewe. Matokeo yanaonesha kuwa mali zote zilichukuliwa na jamaa wa Ndaro ambao waligawana pasipo kumshirikisha Bigeyo.

Hatimaye, Bigeyo aliamriwa kurudi kwao pasipo kuchukua kitu chochote walichokizalisha na mumewe. Mwandishi anasema:

Bigeyo pia alirudi kwao. Yeye pia hakurithi chochote. Kila kitu kilichukuliwa na jamaa za Ndaro. Huo ndio ulikuwa mwisho wa miji miwili (Zakaria na Ndaro) iliyokuwa na mengi ya kuuambia ulimwengu (uk. 97).

Katika dondoo hilo, mwandishi anaonesha mitazamo ya jamii yake kuhusu suala la urithishwaji wa mali kwa wahusika. Kinachojitokeza hapo ni kwamba, licha ya Bigeyo kuishi na mume wake, Ndaro, kwa muda mrefu, jamii yake haioni thamani ya mwanamke huyo na inaamua kumnyang'anya mali zote alizochuma pamoja na mume wake. Kitendo hicho kinamwacha katika mahangaiko kwa kuwa hakuna hata mtu mmoja anayemwonea huruma. Mjane huyu, anaachwa katika mahangaiko kama ilivyo kwa watoto wa Zakaria. Jambo hili lipo katika mazingira halisi ya Waafrika kama wasemavyo Wanasosholojia ya Kifasihi kuwa kazi za kibunilizi ni akiso la maisha halisi ya jamii husika.

Kimsingi, matokeo yanaonesha kwamba mwandishi anatambua thamani ya kurithisha mali kwani mali hizo huweza kumsaidia anayerithishwa katika kutatua matatizo mbalimbali. Hili linathibitika kupitia kwa Regina ambaye anumia mali (ng'ombe) aliorithishwa na baba yake, kuwasomeshea watoto wake, baada ya Zakaria kushindwa kutimiza majukumu yake kama baba wa familia kwa kuendekeza ulevi. Inaelezwa kwamba:

Zamani Zakaria alikuwa mwalimu lakini alifutwa kazi kwa sababu ya ulevi. Jirani zake walisema alijali pombe kuliko watoto: alikuwa hajatoa hata chapa kuwalipia watoto ada ya shule. Kama sasa watoto walikuwa shuleni, heko kwa mama yao. Regina alilima pamba kwa bidii, na pesa alizopata aliwavika watoto wake. Kitu kimoja kilimsaidia sana Regina katika kuelimisha watoto wake – ng'ombe. Baba yake alipokufa, alirithi ng'ombe wanne. Kwa wakati huo wawili walikuwa wamekwishauzwa (uk. 6).

Nukuu hii inaonesha thamani ya mali ya urithi kwani inasaidia kutatua matatizo katika familia kama itatumiwa vizuri. Kwa jumla, mwandishi wa *Rosa Mistika* anakusudia kuonesha kwamba suala la urithishwaji wa mali ni muhimu na halipaswi kuwa la ubaguzi. Hii inatokana na ukweli kwamba Regina licha ya kuwa ni mwanamke, baba yake anamthamini na kumrithisha ng'ombe wanne, ambao hatimaye, wanamsaidia kuihudumia familia yake.

Hitimisho

Makala hii imefafanua mitazamo mbalimbali ya Waafrika inayotumika kama miegamo mikuu katika mchakato wa urithishwaji mali kwa kujiegemeza katika bunilizi za Kiswahili, hususani riwaya zilizoandikwa na mwandishi nguli Euphrase Kezilahabi. Mjadala umetokana na data zilizopatikana kwa njia ya usomaji wa riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975). Pia, mjadala umeegemezwa katika Nadharia ya Wanasosholojia ya Kifasihi. Kwa jumla, matokeo yameonesha kuwa, kwa Waafrika, mchakato wa urithishwaji wa mali hujiegemeza katika mitazamo mbalimbali inayozingatiwa kulingana na maamuzi ya mrithishaji au walithishwaji. Mitazamo iliyojadiliwa katika makala hii ni mitatu, ambayo ni: mtazamo wa kiutamaduni, kihari na kimabavu. Hivyo, inapotokea suala la ugawaji wa mali kwa walengwa, wahusika hujiegemeza katika mtazamo mmojawapo katika zoezi hilo. Hata hivyo, mjadala umeonesha wazi kuwa mtazamo wa kiutamaduni ndio unaotumiwa zaidi na Waafrika katika mchakato wa urithishwaji wa mali. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, maisha ya mwanadamu huongozwa na mitazamo mbalimbali inayokitwa katika misingi ya kitamaduni. Hivyo, kila mmoja huupokea na kuuchukulia mtazamo huu kuwa ni wa kawaida kulingana na uhalisi wa maisha yao.

Marejeleo

- BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.
- Chama cha Wanasheria Tanzania Bara, (2015). *Ijue Sheria ya Uritibi, Mirathi na Wosia: Sheria katika Lugha Rahisi*. Dar es Salaam: Tanganyika Law Society.
- Coser, L. (1963). *Sociology through Literature: An Introductory Reader*. Prentice Hall, Englewood Cliffs.
- Idowu, E. B. (1973). *African Traditional Religion: A Definition*. New York: Obis Books Maryknoll.
- Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Dar es Salaam: EastAfrica Literature Bureau.
- Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Dar es Salaam: EastAfrica Literature Bureau.
- Kezilahabi, E. (1985). African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation (PhD Thesis). University of Wisconsin-Madison, USA.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.
- Mbiti, J. S. (2011). *African Religions and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.
- Merriam, S. B. & Tisdell, E. J. (2016). *Qualitative Research: A Guide to Design and Implementation*. 4th Edition. San Francisco. Jossey-Bass.
- Mlacha, S. A. K na Madumulla, J. S. (1991). *Rivaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mulokozi, M. M. (1983). “Dunia Uwanja wa Fujo (Mapitio ya Kitabu),” katika *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Juz. 50/1, kur 1 – 12. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihili ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Mungah, C. I. (1999). “Dhana ya Maisha katika Novela Mbili za Euphrase Kezilahabi: Nagona na Mzingile”. *Tasinifu ya Kutoshleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya “Masters of Arts” (Hajjachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- National Organisation for Legal Assistance (2006). *Sheria za Uritibi na Wosia*. Dar es Salaam: NOLA.
- Narizvi, S. (1982). *The Sociology of Literature of Politics*. Australia: Edamund Burke.
- Oruka, H. O. (1990). *Trends in Contemporary African Philosophy*. Nairobi: Shirikon Publishers.
- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma Tanzania: Central Tanganyika Press.
- Robert, S. (2013). *Kufikirika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu cha Fasihili Simulizi; kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza Tanzania: Serengeti Bookshop.
- Swai, S. O. (2021). *Mirathi Nchini Tanzania: Mwongozo kuhusu Mirathi, Wosia Na Taratibu Za Kimahakama Tanzania*. Kigoma: Mahakama Kuu
- Temples, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.
- TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharu za Uihakiki wa Fasihili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uihakiki wa Fasihili: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: OpenUniversity Press.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihili Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publication Ltd.